

Moja ya maeneo yenye mvuto zaidi duniani ni eneo la mahusiano, hasa mahusiano yanayopelekea ndoa.

Mahusiano ya uchumba unaopelekea ndoa ni baina ya mvulana na msichana.

Hawa ni watu ambao wanautofauti mkubwa sana kifikra, kimaumbile, kimahitaji n.k, na huo utofauti wao ndio unaotengeneza mvuto wa kutaka kuhusiana.

Pamoja na hivyo lakini

Mahusiano ni eneo ambalo linamigogoro mikubwa na mizito ulimwenguni kote.

kila siku inaibuka migogoro mipya ya mahusiano yenye sura tofauti tofauti ambazo kwa sehemu kubwa hazifurahishi, kiasi kwamba watu wengine wamekufa kwasababu tu ya mahusiano.

Mahusiano yamehatarisha uhai wa watu, yamepoteza na kuua ndoto na maono ya watu.

Mahusiano yamegeuka kuwa kiumbe kinachotishia maisha na chenye ukatili mkubwa juu ya binadamu.

Mioyo ya watu imepasuka inavuja damu na maumivu yasiyoweza kuvumilika, kwa sababu tu ya kitu kinachoitwa mahusiano.

Wanafunzi wameacha masomo, wafanyakazi wameacha kazi, watoto wameacha kuwatii wazazi wao kwasababu tu ya mahusiano.

Katika kitabu hiki nitakupa tips muhimu za kukusaidia kuyaendesha mahusiano yako, uyafurahie zaidi ya unavyotarajia.

Muhimu ni kuyafanyia kazi maelekezo yote nitakayokupa kwenye kitabu hiki.

